

## KUELEKEA SIKU YA MAJI DUNIANI 2023

Mwaka 1993 Umoja wa Mataifa (UN) kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira na Maendeleo lilipitisha Azimio rasmi la kuadhimisha Siku ya Maji Duniani kila mwaka ifikapo tarehe 22 Machi.

Kitaifa, Wizara ya Maji kuanzia mwaka 1988 imekuwa ikiadhimisha Wiki ya Maji kwa kuwashirikisha Wananchi na Wadau wa Maji. Maadhimisho haya yanakwenda sambamba na Azimio Na. 47/193 la Umoja wa Mataifa linalozitaka nchi wanachama kuadhimisha Siku ya Maji Duniani kila tarehe 22 Machi, ambayo kwa Tanzania inakuwa ni kilele cha Wiki ya Maji.

Lengo kuu la maadhimisho ya Wiki ya Maji nchini ni kuungana na Mataifa mengine Duniani katika kutathmini utekelezaji, mafanikio, changamoto na kuainisha mikakati ya kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira na kusimamia utunzaji wa rasilimali za maji nchini. Kaulimbiu ya Siku ya Maji Duniani 2023 ni: **“Kuongeza Kasi ya Mabadiliko katika Sekta ya Maji kwa Maendeleo endelevu ya Uchumi”** na kazi mbalimbali kuelekea Siku ya Maji Duniani zitaongozwa na **Mhe. Kassim Majaliwa** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 16 Machi kwa kuzindua mradi wa maji jijini Dar es salaam.

### **Madhumuni Mahsusi ya Maadhimisho ni;**

- Kuelimisha Jamii na wadau kuhusu Sera ya Maji na majukumu yao katika kuitekeleza;
- Kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa Programu ya Maji; Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji; Hali ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira; na kuweka mikakati ya kuboresha utoaji wa huduma;
- Kuwaleta pamoja wataalamu wa sekta ya maji katika majadiliano, kujifunza na kubadilishana uzoefu;
- Kuhamasisha ubunifu wa kisayansi katika utafiti na teknolojia katika utoaji wa huduma na utunzaji wa vyanzo vya maji;
- Kutathmini mafanikio ya sekta ya maji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita.
- Kuwakutanisha wadau mbalimbali (taasisi binafsi, wadau wa maendeleo na Serikali) katika kubaini fursa za uwekezaji kupitia sekta ya maji; na
- Kutathmini mchango wa sekta ya maji katika tasnia nzima ya maendeleo ya viwanda nchini.

Wizara ya Maji hushirikiana na wadau mbalimbali kutathmini utekelezaji na utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Maadhimisho haya yatafanyika kwa shughuli mbalimbali zinazohusiana na utoaji wa huduma ya maji; utunzaji wa vyanzo vya maji nchini; kupanda miti; kusaini mikataba mikubwa ya miradi ya maji; kutoa elimu kwa jamii na wadau; uzinduzi wa miradi ya maji na usafi wa mazingira pamoja na kuhamasisha ubunifu, tafiti na teknolojia katika sekta ya maji. Aidha, wiki hii itatumika kama wiki maalumu ya Sekta ya Maji nchini kujitathmini kwa kujilinganisha na nchi nyingine Duniani katika kukabiliana na changamoto

zinazoikabili Sekta ya Maji. Sambamba na maadhimisho haya, kwa mwaka huu, Wizara itashiriki katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa unaohusu masuala ya maji “UN 2023 Water Conference”.

### **Shughuli zitakazofanyika kuelekea Siku ya Maji Duniani 2023**

- i. Kongamano la Kisayansi la Sekta ya Maji (Water Scientific Conference) litafanyika tarehe **8 - 10 Machi 2023, Ubungo Plaza Dar es Salaam** na litafunguliwa na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb);
- ii. Uwekaji wa mawe ya msingi; uzinduzi wa miradi ya maji nchini; upandaji miti; kusaini mikataba na kutoa elimu kwa jamii na wadau kupitia nyenzo mbalimbali. Tarehe **18 Machi, 2023** Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatarajiwa kuzindua mradi wa maji wa Orkesumet uliopo wilaya ya Simanjiro mkoa wa Manyara.
- iii. Siku ya EWURA ambapo ripoti ya EWURA ya tathmini ya utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira itazinduliwa na mgeni rasmi Mhe. Dkt. Philip Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe **20 Machi 2023, Dar es salaam**.
- iv. Mkutano wa Mapitio ya Sekta ya Maji (*Joint Water Sector Review*) utafanyika Siku ya Maji Duniani tarehe **22 Machi 2023, Dar es salaam**.